



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 31 Mei, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. **TAARIFA YA SPIKA:**

II. **HATI ZA KWASILISHA MEZANI:**

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka 2024/2025.

Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa Mwaka 2024/2025.

III. **MASWALI:**

Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

222. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe)
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Tathmini ya hewa ya ukaa ipo vipi kwa mustakbali mzima wa mabadiliko ya tabianchi.

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

25. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Ligi ya Muungano ina mchango mkubwa sana katika kuinua mpira wa miguu Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Je, ni lini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kwa kushirikiana na Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT) itairejesha rasmi ligi ya Muungano hapa Zanzibar.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

101. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Vanila ni zao muhimu la viungo linalozalishwa katika visiwa vya Zanzibar na kuingizia Zanzibar fedha za kigeni. Hata hivyo, kwa takribani miaka miwili sasa, soko la vanila limekuwa likiyumba na kuwakatisha tamaa wakulima wa zao hilo amba o wamewekeza fedha na nguvu zao kwa muda mrefu.

- (a) Je, Serikali inalitambua tatizo hili la soko kwa wakulima wa vanila, na ni hatua gani inazichukua katika kuwasaidia wakulima hawa kukabiliana na changamoto za soko.
- (b) Je, ni ipi takwimu halisi za uzalishaji wa vanila na viungo vyengine kwa Unguja na Pemba.
- (c) Je, Serikali ina mkakati gani endelevu wa kuhakikisha mazao ya viungo, ikiwa ni pamoja na vanila, yanapata soko linaloakisi nguvu na jitihada zinazotumiwa na wakulima katika visiwa vyetu.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

56. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali ya Awamu ya Nane chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, imefanya kazi nzuri ya kuimarisha miundombinu ya elimu kwa kujenga skuli nzuri na za kisasa Unguja na Pemba. Pamoja na mazingira hayo mazuri bado skuli zetu haziwapi utulivu wa kujifunza wanafunzi wetu, ikiwa ni pamoja na wanafunzi

kufanyishwa kazi za huduma za majengo ya skuli kama vile usafi na mengineyo.

- (a) Je, kwa nini Wizara yako haiweki utaratibu wa kuajiri kampuni za usafi na huduma nyengine badala ya kuwatumia wanafunzi kufanya kazi hizo.
- (b) Je, Wizara haioni kuwa wanafunzi kufanya kazi za usafi kunawafanya wapate uchovu kabla hawajaingia kwenye vipindi vyta masomo na kusababisha kupunguza morali ya kujifunza.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

255. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tunaipongeza Serikali yetu kwa kusikiliza vilio kwa wananchi wake pale ilipoamua kuwatengenezea barabara ya Finyakicha. Hata hivyo bado inaonekana kama kuna mkwamo hasa kwenye uendelezaji wa barabara hiyo.

Je, ni sababu zippi zilizopelekea kuchelewa kumalizika kwa barabara hii.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

49. MHESHIMIWA MARYAM THANI JUMA (Jimbo la Gando) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

- (a) Je, ni taasisi gani zisizo za kiserikali ambazo Wizara inashirikiana nazo katika kupinga na kuzuia vitendo vyta ukatili wa kijinsia.
- (b) Je, taasisi hizo zina mchango gani katika kusukuma kasi ya kupunguza vitendo hivi.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2024/2025.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka 2024/2025.

Zanzibar,
31 Mei, 2024.



(Raya Issa Msellel)
KATIBU WA BARAZA